TANGAZO LA SERIKALI NA. 48 la tarehe 26/1/2024

SHERIA YA USIMAMIZI NA USHURU WA BIDHAA
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MATANO YA MRADI WA AFYA YANGU WA WIZARA YA AFYA YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye Magari Matano ya Mradi wa Afya Yangu wa Wizara ya Afya ya Mwaka 2024, na itaanza kutumika kutumika kuanzia tarehe 10 Desemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote yanayoweza kuimarishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na magari matano yaliyoanishwa kwenye Jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na Wizara ya Afya kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Afya Yangu, kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini

ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo tarehe 07 Juni, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Namba ya Chasis | Namba ya Injini |
|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71J80F022398 | 1HZ-1026543 |
| 2 | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71JX0F022404 | 1HZ-1026562 |
| 3 | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71JX0F022371 | 1HZ-1026328 |
| 4 | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71J30F022387 | 1HZ-1026446 |
| 5 | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71J90F022409 | 1HZ-1026610 |

Dodoma,
11 Januari, 2024.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*